TANGAZO LA SERIKALI Na. 788 la tarehe 30 SEPTEMBA, 2011

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

CHAPISHWA KATIKA GAZETI LA
Tarehe 30/09/2011

(SURA 290)

SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7 (1) na 16(1)*

# SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO, ~~2010~~ ZA MWAKA 2011

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro za mwaka ~~2010~~ 2011 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:

"Ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa ajili ya huduma, vibali na leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Plinth area" maana yake ni eneo la jengo lililotumika kujenga.

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290.

"Taka" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi mazingira ya Mwaka 2004 maana yake ni kitu chochote kiminiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya haii ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha uharibifu wa mazingira ambayo inajumuisha taka.

"Taka ngumu" maana yake ni taka ambazo hutoka katika umajimaji kutoka majumbani. Katika majengo ya biashara, viwandani na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi plastic au taka laini

zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya maari mabovu (scraps).

"Taka za Viwandani" maana yake ni uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiotokana na uzalishaji viwandani ambao ni chanzo cha nishati, maji, mimea iliyotiwa dawa, au mawasiliano.

"Uchafu Hatari" maana yake ni kitu chochote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani, au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemia, kwa binadamu au mazingira.

"Wakala" maana yake ni mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au Taasisi iliyoteuliwa na Halmashauri kutoa huduma zinazohusiana na Sheria Ndogo hizi.

Ada na ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza na kukusanya Ada na Ushuru kwa ajili ya huduma mbalimbali, vibali na leseni zitolewazo kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na Ushuru utozwao chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupata huduma au leseni au kibali husika.

(3) Ada na Ushuru zitozwazo zitalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake ambaye atatoa stakabadhi yenye Nembo ya Halmashauri kama kielelezo cha kukubali malipo hayo.

Ada ya uzoaji taka

5. (1) Halmashauri itatoza ada ya uzoaji taka kulingana na kiwango cha uzalishaji wa taka

(2) Taka zote zitatupwa katika dampo la Halmashauri kwa kulipia ada na kila Wakala, taasisi za jamii na taasisi nyingine zozote ambazo zitajishughulisha kuzoa na kutupa taka:

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

6. Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayestahili kulipa ada au ushuru kulipa ada na ushuru kama zilivyoelekezwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Udhibiti wa ujenzi

7. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kujenga jengo lolote bila kuwa na kibali cha ujenzi kutoka Halmashauri.

Ukusanyaji wa madeni

8. (1) Endapo mtu yeyote anayetakiwa kulipa ada au ushuru atashindwa kulipa ndani ya muda unaotakiwa kulipa, Halmashauri inaweza kukusanya ada hizo kwa njia ya Mahakama.

(2) Bila ya kuathiri masharti yaliyowekwa na kifungu cha (1) hapo juu, Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ada kwa njia ya kukamata na kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na



21

deni la Ada au Ushuru.

(3) Baada ya siku thelathini (30) kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada. Uwezo wa kuuza mali zilizokamatwa na kushikiliwa utakuwa halali iwapo Mkurugenzi, kwa maandishi atatoa taarifa ya kusudio la kuuza mali hizo endapo mwenye mali atashindwa kulipa deni anaodaiwa pamoja na adhabu ndani ya kipindi cha siku kumi na nne (14).

Uwezo wa Afisa Muidhiniwa

9. Afisa Muidhiniwa anaweza kuingia katika jengo lolote kwa nia ya kukusanya ada au ushuru.

Makosa na adhabu

10. Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mtu yeyote:

(a) atakataa au atakwepa kulipa Ada na Ushuru anaopaswa kulipa

(b) atamshawishi mtu yeyote au kundi la watu wasilipe Ada na Ushuru huo kwa namna yoyote ile bila sababu ya msingi.

(c) akiwa ni wakala akishindwa kuwasilisha kiasi cha Ada au Ushuru alichokusanya na katika wakati muafaka.

Kufifilisha kosa

11. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini nje ya Mahakama iwapo mkosaji kwa hiari yake amekubali kwa maandishi kwa kutumia fomu maalum kulipa faini na kiasi cha Ada au Ushuru anachodaiwa.

12. Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia, atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000.00) au kifungo cha miezi kumi na miwili (12) au vyote kwa pamoja, faini na kifungo.

G.N. No.309

13. (The Morogoro Municipal Council (fees ,and charges) By – Laws, 1999) zimefutwa.

## JEDWALI

### SEHEMU 'A'
### ADA YA USAJILI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1) | Mabasi madogo | ... ... ... | Sh: 15,000.00 kwa mwaka |
| 2) | Teksi | ... ... ... ... ... | Sh: 10,000.00 kwa mwaka |

### SEHEMU 'B'
### ADA YA UZOAJI TAKA

| | | | |
|---|---|---|---|
| a) | Viwanda | ...... | Sh: 120,000.00 kwa mwezi |
| b) | Taasisi | ......... | Sh: 60,000.00 kwa mwezi |
| c) | **Hoteli**: (i) Katikati ya Mji | ......... | Sh: 60,000.00 kwa mwezi |
| | (ii) Maeneo mengine | ......... | Sh: 25,000.00 kwa mwezi |
| d) | Nyumba za kulala wageni na migahawa | ...... | Sh: 20,000.00 kwa mwezi |
| e) | **Viwanda vidogo**: | | |
| | (i) Useremala na gereji | ......... | Sh: 30,000.00 kwa mwezi |
| | (ii) Maeneo mengine | ......... | Sh: 25,000.00 kwa mwezi |
| f) | Hospitali | ......... | Sh: 75,000.00 kwa mwezi |
| g) | Vituo vya mafuta | ......... | Sh: 45,000.00 kwa mwezi |
| h) | **Nyumba za kuishi**: | | |
| | (i) Katikati ya Mji | ......... | Sh: 200.00 kwa siku |
| | (ii) Maeneo mengine | ......... | Sh: 100.00 kwa siku |
| i) | Biashara nyingine | ......... | Sh: 15,000.00 kwa safari moja *(trip)* |
| (j) | Ada ya uzoaji maji taka (asasi) | ......... | Sh: 15,000.00 kwa gari *(container)* |
| (k) | Utupaji taka ngumu kwenye Dampo la Halmashauri | ...... | Sh: 10,000.00 kwa tani |

## SEHEMU 'C'
## ADA YA UNYONYAJI MAJI TAKA KWENYE MASHIMO NA HUDUMA ZA MTANDAO WA MAJI TAKA

1) *Unyonyaji maji taka*:

| | | |
|---|---|---|
| a) Viwandani, Taasisi na Mashirika | .................. | Sh: 25,000.00 kwa safari |
| b) Maeneo ya biashara | .................. | Sh: 25,000.00 kwa safari |
| c) Maeneo ya makazi | .................. | Sh: 15,000.00 kwa safari |

2) Kuzibua mashimo yaliyoziba kwa mita moja kati ya shilingi 1,000.00 na shilingi 4,000.00

3) Kuunganisha mabomba mapya:

| | | |
|---|---|---|
| (i) Makazi | .................. | Sh: 6,000.00 |
| (ii) Viwandani | .................. | Sh: 10,000.00 |
| (iii) Taasisi na Mashirika | .................. | Sh: 8,000.00 |

4) Kukodisha gari la maji taka nje ya Halmashauri shilingi 35,000.00 kwa safari *(trip)* bila gharama za mafuta na shilingi 1,000.00 kwa kila kilomita kwa umbali ambao huduma itatolewa.

## SEHEMU 'D'
## USHURU WA MATANGAZO

1) Kibali cha muziki na disko

| | | |
|---|---|---|
| i) Onyesho la muziki wa dansi | .............. | Sh: 10,000.00 |
| ii) Muziki wa Disko *(Discotheque)* | .............. | Sh: 10,000.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2) | Kibali na ada ya sinema ya kwenye gari na maonyesho ya video | .............. | Sh: 10,000.00 |
| 3) | Kibali na ada ya kutangaza shughuli zilizotajwa hapo juu | .............. | Sh: 20,000.00 kwa siku |
| 4) | Kodi ya burudani asilimia 5 (5%) ya makusanyo ya mlangoni. | | |
| 5) | Maombi ya kuweka Tangazo au kujenga au kutumia jengo kwa lengo la kutangaza | .............. | Sh: 10,000.00 kwa siku |
| 6) | Matangazo yasiyo na taa kwa kila futi mraba moja kwa mwaka | .............. | Sh: 7,000.00 |

7) Matangazo yenye taa kwa kila futi mraba moja kwa mwaka .......... Sh: 10,000.00

8) Matangazo kwa kutumia vipaza sauti .............. Sh: 20,000.00 kwa siku

9) Matangazo kwa maonesho .............. Sh: 15,000.00 kwa siku

10) Matangazo ya kubandika *(poster)* karatasi ya A4 .............. Sh: 500.00 kwa karatasi *(poster)* moja.

**SEHEMU 'E'**

ADA YA HUDUMA NA KUKODISHA

1) ***Huduma ya kupulizia dawa***:
   a) Makazi ......... Sh: 500.00 per $m^3$

   b) Viwandani .............. Sh: 1,000.00 per $m^3$

   b) Upuliziaji binafsi ndani ya Halmashauri .............. Asilimia 20 ya gharama

2) ***Uondoaji magari yaliyotekelezwa***:
   a) Chini ya tani 3 .............. Sh: 50,000.00

   b) Tani 3 hadi 6 .............. Sh: 100,000.00

   c) Zaidi ya tani 7 .............. Sh: 150,000.00

3) Huduma ya chanjo (haihusishi watoto chini ya umri wa miaka 6) .............. Sh: 6,000.00

4) Kukodisha ukumbi wa Halmashauri (semina na mikutano) .............. Sh: 200,000.00 kwa siku

5) Kukodisha viti .............. Sh: 200,000.00 kwa siku

6) ***Ada ya kukodi vifaa na mitambo (bila mafuta)***:
   a) Tipper tani 10 .............. Sh: 120,000.00 kwa siku
   b) Tipper tani 07 .............. Sh: 100,000.00 kwa siku

   c) Lori la mkonga .............. Sh: 80,000.00 kwa siku

   d) Changanya zege .............. Sh: 35,000.00 kwa siku

   e) Fagio la barabara .............. Sh: 40,000.00 kwa siku



30

| | | |
|---|---|---|
| f) Shindiria (roller) | .............. | Sh: 50,000.00 kwa siku |
| g) Greda | .............. | Sh: 500,000.00 kwa siku |
| h) "Wheel roller" tani 10 | .............. | Sh: 250,000.00 kwa siku |
| i) Vibratory roller tani 10 | .............. | Sh: 350,000.00 kwa siku |
| j) "Plate Compactor" | .............. | Sh: 30,000.00 kwa siku |
| k) Chemsha lami (bitumen boiler) | .............. | Sh: 250,000.00 kwa siku |
| l) Sambaza kokoto (chipping spreader) | .............. | Sh: 200,000.00 kwa siku |
| m) "Air compressor CTL" | .............. | Sh: 200,000.00 kwa siku |
| n) "Alpha cutter" | .............. | Sh: 50,000.00 kwa siku |
| o) "Wheel loader" | .............. | Sh: 500,000.00 kwa siku |
| p) Boza la maji | .............. | Sh: 70,000.00 kwa siku |

7) *Ada ya vitega uchumi:*

| | | |
|---|---|---|
| a) Kilabu cha Manzese | .............. | Zabuni |
| b) Kilabu cha Kaloleni | .............. | Zabuni |
| c) Uwanja wa Gofu | .............. | Zabuni |
| d) Bustani ya Mango | .............. | Zabuni |
| e) Bustani ya **"Rock Garden"** | .............. | Zabuni |
| f) Ukumbi, Baa na mgahawa (DDC) | .............. | Zabuni |
| g) "Palm Resort" | .............. | 50,000.00 kwa mwezi |
| h) Ada ya pango vibanda vya Halmashauri: | .............. | Sh: 50,000.00 kwa mwezi |
| i) Vyumba vya kuuzia nyama (Butchery rooms) | .............. | Sh: 30,000.00 kwa mwezi |
| j) Mgahawa – Soko kuu | .............. | Sh: 40,000.00 kwa mwezi |
| k) Vizimba/vikazi (meza) | .............. | Sh: 10,000.00 kwa mwezi |
| l) Vibanda kwenye vituo vya mabasi | .............. | Sh: 30,000.00 kwa mwezi |

m) Vioski – mjini kati ............... Sh. 50,000.00 kwa mwezi

n) Vibanda kwenye maeneo ya umma ukitoa vilivyofafanuliwa hapo juu ............... Sh: 20,000.00 kwa mwezi

## SEHEMU "F"
## USHURU WA MAGULIO

1) Nguo za mitumba ............... Sh: 200.00 kwa siku

2) Viatu vya mitumba ............... Sh: 200.00 kwa siku

3) Wachonga vifaa vya vyuma *(smiths, soldering)* ............... Sh: 200.00 kwa siku

4) Mboga mboga ............... Sh: 200.00 kwa siku

## SEHEMU "G"
## ADA YA VIBALI VYA UJENZI

1) *Ada ya kuhakiki vibali*:

(a) *Nyumba za makazi*:

(i) Eneo 1 – 100 $m^2$ ......... Sh: 30,000.00 kwa kila ramani

(ii) Eneo la 101 – 150 $m^2$ ......... Sh: 45,000.00 kwa kila ramani

(iii) Eneo la 151 – 200$m^2$ ......... Sh: 60,000.00 kwa kila ramani

(iv) Endapo eneo la ujenzi litazidi 200$m^2$, ada itakayotozwa itaongezeka shilingi 300.00 kwa kila mita za mraba 10 zinazoongezeka.

(b) *Nyumba za makazi na biashara*:

(i) Eneo la 1 – 100$m^2$ ............... Sh: 45,000.00

(ii) Eneo la 101 – 150$m^2$ ............... Sh: 65,000.00

(iii) Eneo la 151 – 200$m^2$ ............... Sh: 90,000.00

(iv) Pale ambapo eneo litazidi 200$m^2$ ada itakayotozwa itaongezeka shilingi 450.00 kwa kila mita mraba

itakayoongezeka.

(c) *Majengo ya kuabudia*
Ada itakayotozwa ni shilingi 25,000.00 kwa kila jengo la kuabudia bila kujali ukubwa wa eneo. Ieleweke kuwa, kila jengo la ziada litakalojengwa litalipiwa ada kulingana na matumizi ya jengo husika.

(d) *Maghala*:
**Ada ya majengo ya maghala ni kama ifuatavyo**:

i) Eneo la 1 – 150m$^2$ ......... Sh: 60,000.00

ii) Eneo la 151 – 200m$^2$ ......... Sh: 90,000.00

iii) Eneo la 201 – 300m$^2$ ......... Sh: 120,000.00

iv) Pale ambapo eneo litazidi 300m$^2$ itaongezwa shilingi 6,000.00 kwa kila mita mraba 10.

(e) **Jengo la ghorofa – makazi**:

i) Eneo la ujenzi kwa ujumla 1 – 100m$^2$ ......... Sh: 60,000.00

ii) Eneo la ujenzi kwa ujumla 101 200m$^2$ ......... Sh: 90,000.00

iii) Eneo la ujenzi likizidi 200m$^2$ ......... Sh: 120,000.00

iv) Eneo la ujenzi likizidi 200m$^2$ ada itakayolipwa itaongezeka shilingi 600.00 kwa kila mita mraba 10 zitakazoongezeka.

(f) **Jengo la ghorofa – Biashara**:

(i) Eneo le ujenzi kwa ujumla – mita mraba 1 – 100 (1 – 100m$^2$) ......... Sh: 80,000.00

(ii) Eneo la ujenzi kwa ujumla mita mraba 101 – 150 (101 – 450m$^2$) ......... Sh: 120,000.00

(iii) Eneo la ujenzi kwa ujumla mita mraba 151 – 200 (151 – 200m$^2$) ......... Sh: 160,000.00

(iv) Pale ambapo eneo la ujenzi linazidi mita mraba 200, ada itakayolipwa itaongezeka shilingi 300.00 kwa kila mita mraba 10 zilizozidi.

(g) **Shule**:

(i) Ada ya kibali cha ujenzi wa shule ----------- Shilingi100,000 kwa majengo ya kawaida.

(ii) Ada ya kibali cha kujenga shule yenye ghorofa na sakafu juu ikizidi mita mraba 100 atalipa ada mlingano. Pale ambapo sakafu ya juu itakuwa chini ya mita mraba 100 ada itakayolipwa itakuwa ile ya jengo la kawaida kama (i) hapo juu. ---------- Shilingi 200,000.00.

2) *Ada ya ramani iliyorudishwa au kurekebishwa*: shilingi 25,000.00

(a) Ramani iliyopitishwa ikirudishwa na kazi haikufanyika au maombi yakiletwa kwa ajili ya kuongezewa muda wa kibali kilichokwisha,

(b) Ada ya marekebisho madogo itakayotozwa ni asilimia hamsini (50%) ya ada ya awali iliyolipwa.

(c) Ada ya ramani za ujenzi zilizotayarishwa na Halmashauri:

(i) Nyumba za makazi ya msongamano ......... Sh: 80,000.00

(ii) Nyumba za makazi ya kawaida ......... Sh: 110,000.00

(iii) Nyumba za makazi tulivu ......... Sh: 150,000.00

3) *Ada ya uchapaji*:

(a) **Ramani za rangi**:

(i) Ukubwa wa AO ......... Sh: 30,000.00

(ii) Ukubwa wa A1 ......... Sh: 15,000.00

(iii) Ukubwa wa A2 ......... Sh: 10,000.00

(iv) Ukubwa mdogo usiozidi au sawa na A.3 ......... Sh: 3,500.00

(b) **Line Map**:

(i) Ukubwa wa AO ......... Sh: 15,000.00

(ii) Ukubwa wa A1 ......... Sh: 10,000.00

(iii) Ukubwa wa A2 ......... Sh: 5,000.00

(iv) Ukuwa wa A3 ......... Sh: 2,000.00

(v) Ukubwa wa A4 ......... Sh: 1,500.00

4) Nakala ya *"soft copy"* isiyozidi mwaka 2000 yenye uwiano na 1:2,500 ......... Sh: 30,000.00

5) Nakala ya *"soft copy"* yenye uwiano wa 1:2,500 *(per sqr.km)* ......... Sh: 60,000.00

**Ada ya ukaguzi wa ujenzi:**
(i) Nyumba ya kawaida (kila mita mraba) ......... Sh: 500.00

(ii) Ghorofa (kwa kila ghorofa) ......... Sh: 5,000.00

**Ada ya kubadili matumizi ya ardhi:**
Ada ya maombi ya mabadiliko ya matumizi ya Ardhi haitarudishwa ......... Sh: 15,000.00

## SEHEMU "H"
## ADA YA UZIO NA MAJUKWAA KWENYE ENEO LA UJENZI

1) Ujenzi wa uzio wa mabati kuzunguka eneo la ujenzi kwa muda wa miezi sita (6) kila eneo .............. Sh: 270.00 kwa mita

2) Ujenzi wa uzio wa mabati kuzunguka eneo la ujenzi kwa muda wa miezi saba hadi ishirini (7 – 20) .............. Sh: 300.00 kwa mita

3) Kwa muda unaozidi miezi 20 .............. Sh: 350.00 kwa mita

## SEHEMU "I"
## ADA YA VIBALI VYA KUKATA AU KUZIBA BARABARA

1) Kukata barabara ya lami .............. Sh: 135,000 kwa mita

2) Kukata barabara ya kifusi .............. Sh: 10,000 kwa mita

3) Kukata barabara ya udongo .............. Sh: 7,000 kwa mita

4) Kukata pembezoni mwa barabara

kusikošakatiwa mjini kati (CBD) ............ Sh: 7,000 kwa mita

5) Kufunga barabara kwa ajili ya sherehe na shughuli nyingine ............ Sh. 40,000 kwa siku

**SEHEMU "J"**

USHURU WA MADINI YA UJENZI

1) Tani 1 – 3½ .............. Sh: 1,000.00 kwa safari

2) Tani 4 – 7 .............. Sh: 1,500.00 kwa safari

3) Tani 8 na kuendelea .............. Sh: 2,000.00 kwa safari

**SEHEMU "K"**

USHURU WA MACHINJIO

| **Aina ya myama** | | **Ushuru** |
|---|---|---|
| 1) Ng'ombe | ----- | Sh: 2,000.00 kwa kila ng'ombe atakayechinjwa |
| 2) Mbuzi/kondoo | ----- | Sh: 1,000.00 kwa mbuzi/kondoo atakayechinjwa |
| 3) Nguruwe | ----- | Sh: 1,000.00 kwa kila nguruwe atakayechinjwa |

**SEHEMU "L"**

USHURU WA MNADA

| **Aina ya myama:** | | **Ushuru** |
|---|---|---|
| 1) Ng'ombe | ................. | Sh: 1,500.00 kwa kila ng'ombe atakayeuzwa mnadani |
| 2) Mbuzi/kondoo | ................. | Sh: 1,000.00 kwa kila mbuzi/kondoo atayeuzwa mnadani |



36